Muhtasari na mapendekezo ya sera

Programu ya Afrika
Aprili 2024

Karatasi ya utafiti

# Kufufua uongozi wa Tanzania kikanda na kurejea kwenye jumuiya ya kimataifa

## Vipaumbele katika kujisikimika kwenye sera ya nje


## Muhitasari

- Tanzania katika siku za hivi karibuni imeanza kuchomoza kutoka kwenye kipindi kigumu cha kujitenga kimataifa chini uongozi wa Rais wa zamani hayati John Pombe Magufuli. Kujitenga huko kulikwamisha historia na hadhi ya Tanzania kwenye luba za uongozi barani Afrika. Hata ivyo, mrithi wake, Samia Suluhu Hassan, mara baada ya kuwa rais aliagiza mapitio ya mkakati wa sera ya nje – ikiwa ni wa kwanza baada ya miongo miwili. Mapitio hayo yanatoa fursa ya kuiwezesha Tanzania kurejesha nafasi yake kama kiongozi wa diplomasia na kiuchumi kikanda na kimataifa.

- Kuibuka kwa ushawishi wa kiuchumi pamoja na kukamilisha ujenzi wa miradi ya kimkakati inayovuka mipaka ya nchi - reli na nishati vitahitaji uongozi madhubuti katika juhudi za muunganiko wa kikanda sambamba na udumishaji wa amani na kusuluhisha migogoro.

- Sera ya Tanzania ya wazi ya kushirikiana na wadau wa kimataifa imeshaanza kuzaa matunda katika biashara na uwekezaji. Mifano katika eneo hili ni kama vile kujenga uhusiano na nchi ya Indonesia and Vietnam; kuimarisha mikakati ya ubia, hususan na nchi za Ghuba ya Arabia pamoja na kukarabati uhusiano wa muda mrefu na China, India na nchi za Magharibi.

- Kurejeshwa taratibu kwa uazimaji na sauti ya Tanzania kwenye luba za kimataifa kunaendelea. Hata hivyo, urejeshwaji huu bado haujasimikwa na hatua madhubiti kutoka pale nchi ilipokuwa imejitenga katika kipindi cha hayati Rais Magufuli. Mapitio ya Sera ya nje ya Rais Samia Suluhu Hassan inaweza kujielekeza kwenye fursa za kiuongozi  kwenye changamoto za kidunia ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi, madini nyeti pamoja na ujenzi wa amani.

- Wasiwasi juu uwekezaji kutoka nje bado ni kikwazo katika ubia na wawekezaji wa nje ukichangiwa na ukosefu wa uratibu kati ya malengo ya diplomasia ya kiuchumi pamoja na utawala wa ndani na mabadiliko ya kidemokrasi. Kupuuzia midahalo hususan inayohusu maeneo tata ya uwekezaji kwenye bandari za Tanzania na mwekezaji kutoka nchi za Ghuba- zinahatarisha kulifanya suala hili kuwa gumu zaidi.

- Hatua madhubuti zinahitajika kuweka mipaka ya kiulinzi wa muda mrefu, kuepusha kujitenga tena au kujitoa. Mapitio ya sera mpya inayotarajiwa hayana budi kujielekeza kwenye maono yanayohimiza kujikita zaidi kwenye mawanda mazuri ya kutokuegemea upande wo wote.


Fergus Kell,
Ally Masabo na
Tilmann Feltes

CHATHAM HOUSE

KONRAD ADENAUER STIFTUNG

## Hitimisho na mapendekezo ya sera

Tanzania imenufaika na mafanikio ya awali tangu kurejea kwake kwenye luba za kimataifa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoka kwenye sera ya kujitenga ya mtangulizi wake, ikiwa imepiga hatua katika kujenga uwanda mkubwa na kurejesha kuaminiana na uhusiano wa kimataifa. Uwanda mkubwa wa mahusiano-uliotokana kwa kwa kiasi kikubwa na juhudi za utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan, kumefungua milango ya machagua na kutoa nafasi ya kujenga miradi mikubwa ya kiuchumi kimkakati kwa malengo mahsusi.

**Tanzania imenufaika na mafanikio ya awali tangu kurejea kwake kwenye luba za kimataifa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoka kwenye sera ya kujitenga ya mtangulizi wake, ikiwa imepiga hatua katika kujenga uwanda mkubwa na kurejesha kuaminiana na uhusiano wa kimataifa.**

Hata hivyo, makovu ya kujitenga na jumuia ya kimataifa wakati kwa utawala wa hayati Rais Magufuli hayajaweza kufutika moja kwa moja. Harakati ya kuwekwa kwenye kumbukumbu iliyobuniwa na Rais Jayaka Kikwete wakati wa awamu yake ya pili ya uongozi ilichangia kujitenga baada ya mwaka 2015, huku kumbukumbu ya msimamo wa hayati Rais Magufuli ikiwa bado haijafutika hasa wasiwasi kwenye uwekezaji wa miradi mipya, hatari ya kurejea kwenye kujitenga bado ipo.

Mapitio mapya ya serikali kwenye sera ya nje inatoa fursa ya kupitiwa upya kwa hisia zote hizo. Mapatio yatawekwa wazi kwa kuzingatia yale yaliyoibuliwa katika utafiti huu. Mengi ya masuala hayo ni ya moja kwa moja. Mafaniko ya haraka yanaweza kupatikana kwa kurejea kwenye 'uchumi wa buluu' au mabadiliko ya tabia nchi kwa mfano. Haya ni masuala muhimu yanayohitaji kupewa kipaumbele, lakini katika kuyatafrisiri hakuhitaji ubahatishaji.

Jukumu kubwa la mapitio ya sera ya nje ya Tanzania limesimikwa katika kuangalia maono ya mikakati, utekelezaji na kuyahuisha yote hayo na uratibu madhubuti wa ndani. Ni vema basi mahitaji ya ndani yakawa ndio nguzo ya sera ya nje kwa kuzingatia maono ya mkakati wa maendeleo waTanzania ifipako mwaka 2050; na kuhuisha sera nyingine kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na madini muhimu katika fursa za kidunia.

Linapokuja suala la kikanda, uhusiano wa Tanzania na majirani zake wakiwemo Kenya na Msumbiji umewekwa katika hali nzuri chini yauongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan. Kwa sasa kuna jukwaa la kuimarisha uongozi baada ya kupitishwa kwa mikataba kama vile TETA, kuwa tayari kusuluhisha migogoro na kujiunga na AfCHPR. Hatua hizo zimerejesha nafasi ya Tanzania na historia yake kwenye ukanda; na hivyo kuonyesha mwelekeo wake wa uchumi tarajiwa.

Uwekezaji wa nje kwenye miradi mikubwa ya miundombinu kumewezekana kutokana na diplomasia ya kiuchumi, na inashawishi kundi la wabia wapya kimkakati. Hata hivyo, sintofahamu kuhusu Bandari ya Dar es Salaam, kumeifanya

serikali kuathirika kutokana na kutokuwa wazi na mawasiliano ya faida, hivyo kusababisha kutengana kwa serikali na maslahi ya umma ambayo imechochewa na hatua za kuzima suati pinzani kutoka kwenye makanisa, mashirika ya hiari na vyama vya upinzani.

## Uwekezaji wa nje kwenye miradi mikubwa ya miundombinu kumewezekana kutokana na diplomasia ya kiuchumi, na inashawishi kundi la wabia wapya kimkakati.

Kuwepo na msimamo thabiti wa kutoegemea upande wo wote kwenye diplomasia ya uchumi hakujaweza kuonekana wazi wazi licha ya juhudi ya kujenga upya taswira ya Tanzania kwenye jumuiya ya kimataifa. Rais Samia Suluhu Hassan ameweka wazi kwamba lengo la sera ya nje la Tanzania ni kurejea kwenye nafasi yake ya uongozi kimataifa.[1] Sera iliyo nyoofu bila kigugumizi itakuwa ni hatua kubwa katika kulifikia lengo lake.

Mapendekezo yafuatayo yamelenga kuongoza uogozi wa Tanzania katika kuandaa na kutekeleza sera yake mpya kwenye luba za kimataifa. Hali kadhalika, mapendekezo yanaweza kusaidia kuharakisha kuielewa sera ya nje Tanzania miongoni mwa wadau wake wa nje.

— **Kujitokeza zaidi kwenye uchumi shirikishi wa kikanda.** Tanzania haina budi kutumia fursa zilizopo kwenye ukanda kuwa ndiye kinara wa uchumi mkubwa katika Afrika Mashariki na kusaidia kuinua muonekano wa miradi ya EACOP na SGR. Zaidi ya kuonyesha umahiri wake kwenye mgogoro na Kenya mathalani, vipaumbele viwekwe kwenye kupasisha TEFA na kuidhinisha ushiriki zaidi kwenye TIC katika kuunga mkono vitega uchumi vya Tanzania kwenye ukanda na hata nje ya ukanda.

— **Kuimarisha nafasi yake katika kutatua migogori kwenye ukanda.** Juhudi kama hizo hazijainua tu rekodi ya Tanzania na kuinua sifa ya Arusha kama kitovu cha majadiliano, lakini pia kuinua jina la Zanzibar. Wakati Tanzania ikijiunga na tume ya SADC huko DRC, inaweza kuibua hisia za kugawanya uaminifu wake kwa kujielekeza zaidi kwenye maeneo mengine zaidi ya uanachama wake wa EAC, hususani katika masuala ya bahari, jambo ambalo ni geni katika mikakati yake ya sera ya nje inayoandaliwa sasa.

— **Kurudi kwenye mikataba ya kimataifa ya utawala na sheria,** hususan AfCHPR na OGP. Ili kuweka alama ya kuachana kabisa na sera isiyotabirika ya huko nyuma, Tanzania inatakiwa kuweka alama kwa kufanya mabadiliko kwa kulishirikisha Bunge katika kupitisha azma ya kujitoa kwenye mikataba ya kimataifa.

**1** FIRST Strategic Insight (2022), *Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Kuimarisha Mahusiano, Kukuza Muungano wa Kimataifa*, ripoti, https://firstforum.org/publishing/reports/the-united-republic-of-tanzania-2022.

- **Kuhakikisha mkakati mpya wenye lengo la kushirikiana na kupata uzoefu toka kwa nchi za uchumi wa kati.** Hii inaweza kuwa ni pamoja na kujenga ubia na nchi za Ulaya ya Kati na Mashariki. Lakini pia kujenga uhusiano na nchi za Indonesia na Vietnam. Kwa minajili ya kujenga uhusiano sawia wa kijiografia. Kuna haja ya kuepusha kumkuza mtu binafsi na vile vile kunahitajika kutenganisha Chama Cha Mapinduzi na dola ya Tanzania.

- **Kuhusanisha biashara ya kimataifa na malengo ya muda mrefu ya kiuchumi.** Kuwepo kwa matarajio ya nchi kutoka kwenye uchumi duni (angalia mapendekezo hapo juu), Tanzania inaweza kufikiria jinsi ya kurejesha mchakato wa majadiliano na Umoja wa Ulaya ambayo yanaweza kusaidia kupata msaada katika maeneo ya uchakataji wa madini.

- **Kuchangamkia fursa za uongozi kwenye luba za kimatifa ili kutelekeza misingi ya ushirikiano wa nchi za kusini.** Kwa mfano, Tanzania inaweza kuonyesha nia yake kuomba uanachama usio wa kudumu kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa mara ya kwanza tangu 2006, na hivyo kuonyesha mchango wake kwenye udumishaji wa amani.[2] Kampeni kwenye kiti cha UNSC kuweza kuendana na madai ya kufanyika kwa mageuzi kwenye mfumo wa Umoja wa Mataifa (UN) kwa kuongoza uwakilishi wa Afrika kwa kuzingatia hoja ya Rais Samia Suluhu Hassan.[3]

- **Kuwa muwazi kwenye mikataba ya uwekezaji wa vitega uchumi kutoka nje na kuruhusu sauti zinazopinga kusikika waziwazi pasipo kuzimwa.** Ni vizuri kwa minajili ya kuwa na sera ya nje iliyo wazi, viongozi wa kisiasa kujiepusha kutaka umaarufu wa muda mfupi ikiwa ni pamoja na kupata maoni ya mkakati mpya hasa kuelekea uchaguzi wa 2025. Moja ya funzo kubwa kutokana na sintofahamu ya bandari ya Dar es Salaam ni nguvu kubwa iliyotumika kuzima ukosoaji ambayo inaweza kusababisha kuibuka kwa nadharia inayokatisha tamaa wawekezaji kutoka nje kwenye miradi mikubwa kama vile bandari ya Bagamoyo.

- **Kusimamia kwa vitendo badala ya kelele tupu linapokuja suala la mabadiliko ya tabia nchi pamoja na masuala ya mazingira.** Mkakati wa sera mpya ya nje unatarajia kugusa maeneo kadhaa ya tabia nchi kwa mara ya kwanza. Mapitio haya yasiguse tu maeneo hayo bali yawe ni rejea katika utendaji kwa maafisa wa serikali wanapokwenda kwa midahalo ya kimatifa kama vile EACOP na miradi ya gesi. Kuwepo kwa Mkakati madhubuti wa madini kunaweza pia kwenda sambamba na diplomasia ya kiuchumi mbali ya mabadiliko ya hali ya nchi.

- **Kuonyeshwe utofauti kati ya sera mpya ya nje kutoka ile ya utawala uliopita kwa kuja na msamiati mpya.** Kupata mafanikio, mkakati mpya lazima uonyesha mwanzo mpya na kuachana na tabia ya kusita sita au wasiwasi

---

**2** Tanzania imetumikia mihula miwili ya uanachama wa UNSC hapo awali, mwaka 1975–76 na 2005–06. Wakati wa awamu ya kwanza kati ya hizo, iliongoza mapambano ya ukombozi wa Afrika, wakati ya pili, ilizingatia masuala ya eneo la Maziwa Makuu. Tazama Shule (2014), 'Kutoka Kusini mwa Afrika hadi Ukanda wa Maziwa Makuu: Changamoto kwa Sera ya Kigeni ya Tanzania na Utatuzi wa Migogoro katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara', Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Newcastle, Australia, http://ogma.newcastle.edu.au:8080/vital/access/manager/Repository/uon:15179.
**3** Business Standard (2023), 'India, Tanzania kufanya kazi pamoja katika mageuzi ya UNSC kupitia upanuzi: MEA', 9 October 2023, https://www.business-standard.com/india-news/india-tanzania-to-work-together-on-reform-of-unsc-through-expansion-mea-123100900702_1.html.

wa uhusiano wa nje. Kukumbatia tu mkakati mpya wa diplomasia ya uchumi na kutofungamana na upande wo wote ilihali kinachoongezeka ni maneno tu, kunaweza kukatisha tamaa. Rejea mifano ya Zambia yenye kufuata '*diplomasia chanya ya kutoegemea upande wo wote*', India yenye '*diplomasia ya upatanishi*' na Malaysia '*diplomasia ya usawa*' ambapo yote inaonyesha mwelekeo sahihi katika hili.[4]

**4** Tazama, kwa mfano, Vandome, C. (2023), *Zambia inayostawi mahusiano ya kimataifa: 'Positive neutrality' na ushirikiano wa kimataifa*, Ripoti, London: Royal Institute of International Affairs, https://doi.org/10.55317/9781784135553.

## Toleo kamili la ripoti

https://www.chathamhouse.org/2024/04/reviving-tanzanias-regional-leadership-and-global-engagement

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kunaswa tena au kusambazwa kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, kielektroniki au kimakanika ikijumuisha kunakili, kurekodi au kuhifadhi taarifa au mfumo wa kurejesha, bila idhini ya maandishi ya awali ya mwenye hakimiliki. Tafadhali elekeza maswali yote kwa wachapishaji.

Chatham House haitoi maoni yake yenyewe. Maoni yaliyotolewa katika chapisho hili ni wajibu wa waandishi.

Copyright © The Royal Institute of International Affairs, 2024

Chapisho hili limechapishwa kwenye karatasi iliyoidhinishwa na FSC.
designbysoapbox.com